

»Ufugaji wa kuku wa nyama kwa uwekezaji mdogo«

Ufugaji wa kuku ni biashara ya kawaida barani Afrika huku kuku wa nyama wakifugwa kwa ajili ya kutoa nyama.

Unapo jenga banda la kuku, mwelekeo ni muhimu sana. Inashauriwa kujenga banda kwenye mwelekeo wa mashariki-magharibi. Hii husaidia jua kuwa juu ya paa ili kuepu ka jua moja kwa moja kwenye banda la kuku.

Mapendelezo ya banda la kuku

Unapo jenga banda la kuku, jenga ukuta imara wenye urefu wa nusu mita kutoka ardhini. Kisha ongeza nyavu kutoka ukuta kwenda juu. Kwa upana, jenga ukuta imara kutoka chini hadi juu.

Bandika mchanga kwenye ukuta ili kurahishisha ushafishaji na kuua vijidudu kwa urahisi. Nyavu uliotumiwa unapaswa kuwa na kipenyo cha mm 10 ili kuzuia ndege na panya wasiingie kwenye banda la kuku kwa sababu hawa hueneza ugonjwa.

Ikiwa banda la kuku tayari limejengwa likielekea upande wa kaskazini-kusini, weka kivuli au paa juu talo ili kuzuia jua ya moja kwa moja kuingia kwenye banda.

Usimamizi wa vifaranga

Kwa matandiko, ni bora kutumia maranda ya mbao kwa sababu haya hunyonya unyevu, na yakinumiwa kwa kina cha sentimeta 10 huwapa vifaranga faraja na pia husaidia kudumisha joto katika banda.

Vifaranga wanapomwaga maji kwenye banda, toa matandiko yaliyoloweka na uweke mapya.

Vifaranga wanavyokua, panua urefu wa vihori vya kulishia na kunyweshea ili kuhakikisha vifaranga wanakula na kunywa kwa urahisi. Pia toa nafasi ya kutosha ya kulishia na kunyweshea vifaranga ambayo ni kihori kimoja cha kulishia na kimoja cha kunyweshea kwa kila vifaranga 50 ili kuepuka ushindani.